# Pesa za Janga la COVID-19 na Msaada wa Vocha ya Mazingatio ya Ulinzi

**- Aprili 2020, itakayosasishwa mara kwa mara**

---

Mwongozo huu kuhusu Msaada wa Pesa na Vocha (CVA) wa Matokeo ya Ulinzi katika kipindi cha janga la COVID-19 umetayarishwa kwa kuzingatia maoni kutoka kwa washiriki wa Timu ya Kazi ya GPC kuhusu Pesa za Ulinzi. Umekusudiwa kuwa kifaa cha marejeleo ya haraka ili kutegemeza CVA na wafanyakazi wa ulinzi wanaofanya kazi moja kwa moja na wateja waliohamishwa na wenyeji kushirikiana katika matumizi ya CVA kwa matokeo ya ulinzi. Mwongozo huu unashughulikia: **(1) CVA kwa matokeo ya ulinzi ndani ya sekta ya ulinzi na; (2) Kuhakikisha CVA imefikishwa salama na kutumika kwa matokeo ya ulinzi ndani ya sekta ya ulinzi.** Hati hii itasasishwa mara kwa mara na italenga kupanua uwezo wake kadiri muda unavyosonga. Inapaswa kusomwa pamoja na mwongozo wote wa COVID-19 wa Global Protection Cluster, ikijumuisha Hatua Zinazohusiana na Itikio la COVID 19 na Utayari wa GPC - Mwongozo wa Programu ya Ulinzi na pia mwongozo wa jumla uliopo kuhusu Ulinzi kupitia Msaada wa Pesa.

---

***Pesa kwa ajili ya Ulinzi*** *ni neno linalotumiwa kufafanua matumizi ya pesa na msaada wa vocha katika kusaidia kufikia matokeo ya ulinzi.*

## Mambo Muhimu ya Kuzingatia ya COVID-19 na CVA ya Ulinzi

**CVA ina uwezo wa kutegemeza matokeo ya ulinzi kwa:**

- Kufikia watu wenye uhitaji haraka na kwa gharama ya chini kuliko aina nyingine za msaada wa dharura.
- Kuwategemeza watu ambao wamefichua visa vya ukatili na wamepatwa na hatari za ulinzi zinazotokana na COVID-19 kupona, ikijumuisha kupata huduma muhimu.
- Kuwategemeza watu/familia ambazo anayekimu mahitaji ya familia anajitenga/anadumisha umbali na watu wengine na/au amepoteza kazi na/au shughuli zinazoleta mapato na wako katika hatari kubwa ya kujihusisha na njia mbaya za kukabiliana na matatizo(kama vile utumikishaji wa watoto, ngono ya biashara, nk. au anaweza kukabiliwa na hatari zilizoongezeka za au kutishiwa kufurushwa.
- Kutegemeza itikio kuelekea kuongezeka kwa hatari ya dhuluma nyumbani kwa sababu ya kuongezeka kwa mikazo ya kiuchumi, kijamii na kiakili kutokana na janga la sasa la COVID-19 na vizuizi vya usafiri vinavyohusika
- Kutegemeza familia ambazo zimewakaribisha watu zaidi wanaowategemea, ikijumuisha watoto, katika makao yao kwa sababu ya familia kutengana.
- Kudumisha mitandao ya kijamii na mifumo ya kutegemeza - ambayo inapofika hupunguza hatari za ukatili kwa watu waliotengwa, kama uwezo wa kupata mawasiliano (kama CVA ili kununua vifaa vya mawasiliano au mkopo wa simu) kati ya washiriki wa familia waliotengana (kwa mfano watunzaji wanapotenganishwa na watoto), na kutegemeza ulinzi wa wafanyikazi walio katika

mstari wa mbele katika kutoa msaada wa kibinadamu, kama vile wafanyikazi wa kesi za ulinzi, au watendaji wa afya.

- Kuandaa fursa ya kuboresha misaada ya kibinadamu ili mapengo ya awali katika huduma-nyeti za umri-jinsia na ulemavu ziweze kushughulikiwa ili zisidhuru na kuboreka kwa watu walioathiriwa na janga.

**CVA ya matokeo ya ulinzi ndani ya itikio la COVID-19 inapaswa:**

- Kutengenezwa kwa kutegemea uchanganuzi thabiti wa hatari na faida za ulinzi hususa wa CVA katika janga la COVID-19. Uchanganuzi huu unapaswa kutegemea utambuzi wa kibinafsi wa mahitaji ya ulinzi na faida ya watu walioathiriwa. Mashauriano yanapaswa kuchukua hatua za tahadhari zinazohitajika ili kuunga mkono miongozo ya afya ya umma, kila inapowezekana kufanyika pasipo kukutana ana kwa ana.
- Ili kuwezesha CVA kutoa matokeo ya Ulinzi, ni muhimu kuelewa hatari zilizopo za ulinzi na ukiukaji,vilevile zile zilizozidishwa au kutokezwa na janga la COVID-19 (kama mikakati hatari ya kukabiliana na matatizo, unyanyasaji wa watoto, unyanyasaji wa kingono na dhuluma ya kingono). Hii inajumuisha hatari za ulinzi zinazohusiana na ugonjwa wenyewe, vilevile hatari ambazo ni matokeo ya hatua zilizochukuliwa (au kutochukuliwa) ili kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo.
- Kuonyesha uchanganuzi thabiti wa muktadha, nguvu, jinsia na jinsi vipengee vinavyopishana vya utambulisho(kama vile umri, mwelekeo wa kijinsia, uwezo, kabila, lugha, dini au asili, n.k.) vinavyoweza kusababisha kutengwa, ubaguzi, uonevu, kuondolewa na ukiukaji wa ulinzi na jinsi CVA inaweza kupunguza au kuzidisha masuala haya ya ulinzi; hatari hizi na visa vya ukatili vitazidishwa na janga la COVID-19 na kuwaathiri vibaya wale waliotengwa zaidi. Uchanganuzi huu unapaswa kufanya zaidi ya kutambua idadi ya kawaida ya "walio hatarini".
- Kutekelezwa kwa njia ambayo inapunguza vizuizi vya ufikiaji kwa idadi ya watu walioathiriwa na inayopunguza kadiri iwezekanavyo mgusano wa watu ili kusaidia kukomesha kuenea kwa ugonjwa huu. Suluhu mbadala za kidijitali na za mbali, kama kutuma pesa kutumia simu na kutegemeza usimamizi wa kesi kupitia simu, zinapaswa kutumiwa kupunguza uwezekano wa maambukizi.
- Kufuatiliwa kwa uangalifu ili kuhakikisha kuwa marejeleo na uhamisho wa CVA kwa kesi za ulinzi zinasaidia kutatua masuala ya ulinzi kama ilivyokusudiwa na haziwaweki wapokezi kwa hatari zaidi. Weka uchunguzi wa faida za ulinzi zilizotambuliwa katika programu za michakato ya uchunguzi na uchunguzi wa baada ya usambazaji (PDM) au vifaa kama hivyo.

## Hatua muhimu Kutumia CVA kuchangia kwa Matokeo ya Ulinzi Katika Maeneo ya Uwajibikaji (AoRs)

- Tumia njia mbalimbali kutambua kesi za ulinzi. Kwa mfano, marejeleo kati ya watendaji wa usimamizi wa kesi, watendaji wa WASH au watendaji wa afya; marejeleo kupitia mitandao iliyopo ya kufikia jamii, nambari za simu na Mashirika ya Walemavu (DPO)
- CVA inayolenga kuchangia matokeo mazuri ya ulinzi inapaswa kutengenezwa wakati wote kama sehemu ya muktadha hususa wa vipengee anuwai ndani ya programu ya ulinzi mpana, kama vile lakini sio tu usimamizi wa kesi, na kuongozwa na wataalamu wa Ulinzi kwa ushirikiano wa karibu na watendaji wa CVA.
- Badili vigezo vya udhaifu kwa msingi wa mabadiliko ya udhaifu na hatari za ulinzi wakati wa janga la COVID-19.

- Fikiria iwapo CVA itasaidia kuunda faida za ulinzi kwa watu walioathirika na ulinganishe hatari na faida za pesa, vocha, vitendo, na bila msaada wa vitu, k.v. kupunguza msaada kwa utetezi wa kisheria au huduma. Fikiria kuhusu jinsi ya kubadilisha kiingilio cha kesi na tathmini za marejeleo ya CVA kwa muktadha wa mbali kupitia simu (ikiwa mitandao inaruhusu); au sivyo fanya tathmini katika jengo lenye uwezo wa hali ya juu wa kuingiza hewa au mahali salama na faragha nje, ikiwa ni lazima.
- Katika hali ambazo CVA inaonekana kuwa yenye kustahili, hakuna "njia moja inayofaa hali zote" kwa mbinu za utoaji, kiasi, muda na ukawaida wa CVA ya ulinzi katika kipindi cha itikio la COVID-19, au itikio lingine lolote; msaada unapaswa kulengwa ili kuhakikisha unafikishwa salama kwa vikundi mbalimbali vya wafadhiliwa kwa kuzingatia msimamo na mwongozo wa pamoja kutoka kwa wataalamu wa ulinzi na watendaji wa CVA.
- Uwasilishaji wa CVA unapaswa kupunguza uhitaji wa watu walioathirika kuondoka manyumbani mwao kuchukua na kutumia CVA; wazee, watu wenye ulemavu na watu walio na matatizo ya kiafya watakuwa katika hatari kubwa ya magonjwa na vifo ikiwa watalazimika kusafiri kuchukua na kutumia CVA. Usambazaji wa nyumba kwa nyumba ambao unazingatia mbinu ya kuokoa, kudumisha kutokujulikana na usiri unapaswa kupewa kipaumbele. Njia za uwasilishaji, kama kutuma pesa kupitia simu, ambazo hupunguza ukaribu, zinapaswa kutumika kila inapowezekana.
- Fikiria vipengee vya kijinsia (kama vile uwezo wa wanawake na wasichana waliobalehe kufikia teknolojia na masoko uhuru wa kusafiri, nyakati za siku zilizotengwa kwa ajili ya kazi ya utunzaji, amri ya kutotoka nje, nk) wakati wa kuzingatia nyakati na maeneo ya usambazaji wa CVA.
- Ili kutumia CVA kwa matokeo ya ulinzi, rasilimali zinazofaa za kifedha na wafanyakazi zinahitajika. Jumuisha mapema CVA kwa matokeo ya ulinzi ndani ya mapendekezo ya ufadhili na maamuzi ya wafanyikazi.
- Hakikisha rasilimali na wakati wa kuwazoeza washikadau muhimu (fikiria kuboresha uwezo wao kutoka mbali, usimamizi wa mbali, matumizi ya teknolojia, n.k.).
- Hakikisha ulinzi wa data na uzingatiaji wa itifaki za kushiriki data na kuhifadhi data unaporejelea kesi za ulinzi za CVA.
- Usambazaji wa habari unapaswa kutengenezwa kulingana na kanuni za muundo za ulimwengu na ziwe zenye kujumuisha kadiri iwezekanavyo, na kupitia njia nyingi. Wazee, watu wenye ulemavu na wasemaji wa lugha zilizo na watu wachache watakabiliwa na changamoto za kupata habari kuhusu programu ya CVA na wanaweza kuwa katika hatari ya kutengwa.
- Njia nyeti ya kuepuka mizozo inapaswa kutumiwa kupunguza hatari ya kuongezeka kwa mivutano ya kijamii ambayo inaweza kuongezeka kutokana na janga.

## Vidokezo Hususa vya AoR

**Dhuluma za Kijinsia.(GBV):**

- Hakikisha kwamba wafanyikazi wanaostahili wa GBV (k.v wafanyakazi wa kesi) wanafanya tathmini za usimamizi wa kesi moja-moja ili kutambua jinsi CVA inavyoweza kusaidia kutatua GBV; wanatathmini mara kwa mara mahitaji na hatari za waathirika na kufanya marejeleo ya CVA yasiyojulikana na ya siri, inapofaa.
- Andaa CVA kwa matokeo ya GBV (k.m IPV, dhuluma ya kinyumbani, ndoa za mapema, SEA, nk) kama sehemu ya muktadha hususa wa huduma anuwai kutegemeza itikio la GBV (mfano usimamizi wa kesi, utoaji wa huduma bora, shughuli za mabadiliko ya tabia, kutengeneza sera na utetezi wa

kisheria) .

- Kuratibu kufungwa kwa marejeleo ya CVA kati ya wataalamu wa GBV na watendaji wa CVA kufikia mkakati wa kuondoka kwa CVA katika kila kesi;
- Fuatilia kwa uangalifu CVA kwa itikio la GBV ndani ya kifurushi cha huduma na usaidizi. Ufuatiliaji wa matokeo unapaswa kuzingatia matokeo yafuatayo: kupunguzwa kwa hatari ya mfiduo kwa GBV (k.m kupunguzwa kwa IPV); kupunguza mikakati hatari ya kukabiliana na matatizo (k.v. kupunguza kazi ya ngono kama mkakati wa kukabiliana na matatizo au kujihusisha na kazi ya ngono kwa njia salama kuliko awali); au upatikanaji wa huduma (km. kuboreshwa kwa uwezo wa kupata huduma za afya ya uzazi), kwa uwiano na malengo ya programu. Matokeo nyeti (kama vile zile mbili za awali) yanapaswa kufuatiliwa tu na wafanyikazi wa kesi au wataalamu wa GBV.
- Kusambaza ujumbe kuhusu huduma za kukabiliana na GBV katika maeneo ambayo huduma za kukabiliana na GBV zimeanzishwa peke yake;tengeneza ujumbe/mpango kwa kushirikiana na wataalamu wa GBV. CVA - na programu ya ajira, zinaweza kuwa sehemu muhimu za kuanzia za usambazaji wa habari kuhusu huduma za itikio la GBV, na maoni yaliyopokewa kuhusu usaidizi salama na unaoweza kupatikana.

*Imetolewa kwa The Cash and GBV Compendium* na*GPC-IASC Identifying & Mitigating Gender-based Violence Risks within the COVID-19 Response Tip Sheet*. Pia tazama GPC Gender-Based Violence And Cash-Based Interventions Tip-Sheet

**Ulinzi wa Watoto (CP):**

- Hakikisha kwamba wafanyikazi wanaostahili wa CP (kama vile, wafanyikazi wa kesi) wanaongoza CVA kwa matokeo ya CP na kufanya tathmini za kibinafsi ili kutambua jinsi CVA inavyoweza kusaidia kusuluhisha mahangaiko ya CP.
- Tathmini kwa ukawaida mahitaji na hatari za CP katika kiwango cha mtoto binafsi na cha familia.
- Toa msaada wa CVA na NFI kwa familia zilizo na watoto ambao fursa zao za kuchuma mapato zimeathiriwa na COVID-19 ili kupunguza utegemezi kwa mikakati hatari ya kukabiliana na matatizo.
- Rejelea kesi za CP kwa CVA, bila kujulikana na kwa busara, inapofaa, kulingana na miongozo ya usimamizi wa kesi ya CP ya janga la COVID-19 (inayokuja) kwa kushirikiana na miongozo maalum ya wakala.
- Endelea kufuatilia mitindo ya muktadha wa CP kwani hizi zitabadilika wakati wa janga; ratibu pamoja na watendaji wa CVA kutia alama maeneo mapya ya kijiografia au vigezo vya kulenga kusawazisha utoaji wa pesa kwa watu waliolengwa au kwa jumla.
- Fuatilia kwa uangalifu marejeleo ya CVA kwa matokeo ya CP ndani ya kifurushi kikubwa zaidi cha huduma na usaidizi. Ufuatiliaji wa matokeo unapaswa kuzingatia upunguzaji wa hatari ya mfiduo kwa mahangaiko ya CP (kwa mfano kupunguzwa kwa ajira ya watoto, dhuluma, n.k.).

Rasilimali nyingine maalum za CP zilizobadilishwa kwa ajili ya janga la COVID-19 zinaweza kupatikana kupitia ukurasa wa Muungano wa CP: Protection of Children during the COVID-19 pandemic. Ona GPC Child Protection and Cash-Based Interventions Tip-Sheet kwa vidokezo zaidi.

**Makazi, Ardhi na Mali (HLP):**

- Toa msaada wa fedha bila masharti ili kuzuia kufurushwa mara moja kwa muda mfupi. Kufurushwa kutaongezeka na kutazidisha hatari ya maambukizi kati ya pande zote zinazohusika katika mchakato wa kufurushwa, vilevile washiriki wengine wa familia na jamii.
- Andaa CVA ili kusaidia huduma zisikatwe kwani familia hazina uwezo wa kuendelea kulipa
- Andaa CVA ili kuhakikisha kwamba familia zinaweza kupata huduma za mitaa, vifaa, vituo, na miundomsingi ambayo inachangia haki yao ya kuwa na makazi yanayotosheleza mahitaji yao
- Hakikisha kwamba CVA inayotolewa kwa wapangaji inawasilishwa pamoja na habari, ushauri nasaha, na usaidizi wa kisheria *uliojumuishwa* na juhudi za utetezi wa kisheria ambazo zinalenga wamiliki wa nyumba na mashirika ya serikali kuhusu kusitishwa kwa kufurushwa na kukatishwa kwa huduma.
- Tumia kuhamisha kama namna ya mwisho wakati kufurushwa hakuwezi kuepukika au kuna hatari kubwa inayohusiana na watu kuishi katika nyumba zao za sasa na kuhakikisha mipango mbadala ya kuandaa nyumba mpya, pamoja na msaada wa kifedha.
- Tazamia ongezeko la kesi zinazohitaji msaada wa kifedha wa haraka, ushauri-nasaha na utegemezo wa kisheria kwa sababu ya mizozo ya urithi na vifo vilivyosababishwa na COVID-19.

Imetolewa kwa*HLP in COVID - Global HLP AOR (Working Document)* na *GPC HLP and CBI Tip Sheet*;

## Hatua Muhimu: Kutambua na Kupunguza Hatari za Ulinzi Zinazohusianishwa na CVA Ambayo Imeundwa Kuchangia Matokeo ya Ulinzi

CVA sio hatari zaidi kiasili kuliko mbinu nyingine za usaidizi (k.v. vitu). Hatari za ulinzi zinazohusishwa na kuanzishwa kwa CVA zinahusiana na muktadha, umri, jinsia na tofauti za watu Kutambua mapema hatari zozote zinazohusiana, kupunguza hatari hizi na ufuatiliaji wa hatari zinazoonekana na mafanikio ya mbinu za kupunguza, ni muhimu katika kuhakikisha kuwa watu walioathiriwa wanaokusudiwa kufaidika na CVA hawapatwi na madhara.

Ili kupunguza hatari na kuongeza faida:

- Tumia kipimo cha umri, jinsia na tofauti za watu katika tathmini, kulenga, muundo, utekelezaji, ufuatiliaji na uwajibikaji.
- Fikiria ikiwa CVA itatokeza au kuzidisha hatari na faida za ulinzi kwa watu binafsi, familia na jamii, na ni kwa kiwango gani hatari mpya zinaweza kupunguzwa na watu walioathiriwa, jamii, mashirika ya kibinadamu na wanaowajibika (serikali) na/au na shughuli za programu za ziada.
- Linganisha hatari na faida za pesa taslimu, vocha, vitu, na kutokuwepo kwa msaada halisi, k.v. kupunguza msaada kwa utetezi wa kisheria au huduma.

Global Protection Cluster

- Linapoonekana kuwa jambo linalopatana na akili kuendelea na CVA, anzisha mbinu za kupunguza hatari na uhakikishe kwamba zina uwezo wa kuwiana na hali mpya (CVA na/au ya vitu) na mbinu za uwasilishaji zinazoweza kubadilikana na hali (kwa mfano kutuma pesa kupitia simu, pesa taslimu mkononi) sio tu kuboresha matatizo yanayoweza kutokana na mifumo ya usambazaji/mfumuko wa bei/usalama, lakini pia mapendezi ya wafadhiliwa - ambayo yanaweza kubadilika wakati wa janga.
- Wafanyakazi wa Fedha na Ulinzi wanapaswa kufanya kazi pamoja na kujishughulisha kupitia vikundi vinavyohusika katika ngazi za mitaa, kitaifa, kikanda na ulimwengu ili kuwasiliana, kushirikiana na kupata taaluma za ziada, haswa wakati wa utathmini, muundo na ufuatiliaji na uchanganuzi. Jumuisha maswali ya ulinzi wa kiwango cha chini katika kipindi chote cha programu.
- Wazoeze wafanyikazi na washiriki wa CVA kuhusu huduma ya kwanza ya kisaikolojia, kuzuia dhuluma ya kingono na unyanyasaji na ulinzi wa watoto, ikijumuisha njia za kurejezewa kwa huduma za ulinzi na kisaikolojia.
- Shughulikia vizuizi vya habari katika programu ya CVA. Usambazaji wowote wa habari unapaswa kuundwa kulingana na kanuni za muundo wa ulimwengu na zenye kujumuisha kadiri iwezekanavyo,na kupitishwa kupitia mbinu nyingi. Wazee, watu wenye ulemavu na wanaozungumza lugha zilizo na watu wachache na vikundi vingine vilivyotengwa watakabiliwa na changamoto kupata habari kuhusu programu ya CVA na wanaweza kuwa katika hatari ya kutengwa.
- Anzisha mfumo wa uwajibikaji, sio tu kwa kipengee cha programu za CVA, ikijumuisha malalamiko kupitia chaneli nyingi na mbinu za kutoa maoni.
- Fikiria ulinzi wa data ya kibinafsi na hatari za kushiriki data za wafadhiliwa na watendaji wa serikali na/au sekta ya kibinafsi, na ujumuishe kanuni za ulinzi wa data katika kipindi chote cha programu.

*Tazama ERC Tips for Protection in Cash-Based Interventions na GPC-IASC Identifying & Mitigating Gender-based Violence Risks within the COVID-19 Response Tip Sheet kwa hatua zaidi.*

---

Kwa kuongezea vile vilivyojumuishwa hapo juu, hapa kuna viunganishi vingine muhimu:

## CBI NA MWONGOZO WA ULINZI NA VIFAA

- Guide for Protection in Cash-based Interventions. Pia inapatikana kwa: FR
- Tips for Protection in Cash-based Interventions. Pia inapatikana kwa: FR
- Key Recommendations for Protection in Cash-based Interventions. pia inapatikana kwa: FR
- Child Safeguarding in Cash Transfer Programming
- Sphere Standards for COVID-19 Responses
- CaLP's Programme Quality Toolbox
- CaLP's thematic web page on CVA within the protection sector
- CaLP's live CVA and COVID-19 guidance inapatikana kwa Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa na Kihispania
- Compilation of CVA and COVID-19 Key Resources from the Cash Learning Partnership (CaLP)
- CaLP's thematic webpage on gender and inclusion
- The Cash and GBV Compendium (kiunganishi kinajumuisha Kiingereza, Kifaransa, Kihispania na Kiarabu.

---

- Mtaala kamili wa kuzoeza wa Pesa Taslimu na GBV katika Kiingereza, Kifaransa, Kihispania na Kiarabu.
- WRC-IRC-Mercy Corps' Cash and GBV Toolkit (Kifaransa, Kiarabu na Kihispania inapatikana pia)
- GPC Mine Action And Cash-Based Interventions Tip-Sheet
- Rasilimali za IRC CVA - Mabadiliko na Itikio la COVID-19: Adaptation Guidance, Distribution Guidance; na Response Guidance;
- Mwongozo wa WFP wa Cash-Based Transfers in the Context of the COVID-19 Outbreak